# Karatasi ya kwanza 102/1

## Insha za kiuamilifu

1. Andika mahojiano baina ya mkuu wa wilaya na mwandishi wa habari kuhusu utovu wa usalama wilayani mwako.

2. Hali ya usalama imekuwa ikizorota katika lokesheni yako. Andika barua kwa chifu wa eneo lenu ukionyesha visa vya ukosefu wa usalama na upendekeze njia za kukabiliana na hali hiyo.

3. Umealikwa katika ofisi ya mkuu wa wilaya kupendekeza njia za kukomesha uadui unaotokana na ukabila nchini. Andika mazungumzo jinsi yalivyoendelea.

4. Wewe ni kiranja anaye husika na masomo shuleni mwako. Mwandikie kiranja anayehusika na masomo katika shule jirani ukiwaalika wanafunzi wake katika mjadala shuleni mwako. Ambatanisha ratiba itakayofuata siku hiyo.

5. Kitengo kinachohusika na usalama barabarani kimekuchagua wewe kama mwanajopo kati ya wanachama watano. Mmetakiwa kuchunguza kinachosababisha ajali nyingi nchini na kutoa mapendekezo yenu jinsi ya kurekebisha hali hiyo. Andaa ripoti yenu.

6. Umehudhuria mkutano wa vijana kujadili njia za kuboresha maisha ya vijana katika jamii. Andika kumbukumbu za mkutano huo.

7. Umefikishwa hospitalini ukiugua. Andika mahojiano kati yako na daktari

8. Wewe ni Afisa Mkuu wa Polisi wilayani mwenu; Andika kumbukumbu za mkutano wa kamati ya usalama uliofanyika hivi karibuni kuhusu mikakati ya kuimarisha usalama wilayani humo.

9 Suala la ufisadi limekuwa tatizo sugu katika jamii ya Kenya. Andika mahojiano kati ya mwenyekiti pamoja na Afisa wa Sheria katika Tume ya Kupambana na Ufisadi nchini na mwandishi wa habari juu ya mbinu za kupambana na ufisadi.

10. Mkuu wa mkoa wa Tuinuane ameongoza mkutano wa viongozi mkoani uliojadili kuhusu amani na maridhiano baada ya vita vya kikabila mkoani humo. Andika kumbukumbu za mkutano huo

11. Matokeo ya mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne yametangazwa. Imesadifu kwamba wewe ndiye mwanafunzi bora katika Mkoa wa Magharibi. Mwanahabari wa Gazeti la Tujivune amekutembelea nyumbani kwenu. Andika mahojiano yenu.

12. Wewe ni Katibu wa kamati ya chama cha wazazi na walimu shuleni mwenu. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanyika hivi karibuni.

13. Kumetokea mzozo wa kisiasa nchini mwako. Mmealika msuluhishi kutoka nchi jirani. Andika mahojiano baina ya msuluhishi huyo na mwanasiasa.

14. Shule yenu ilishiriki hivi majuzi katika mashindano ya riadha ya shule za Sekondari wilayani. Ulikuwa mmojawapo wa washiriki. Andika ripoti kuhusu mashindano hayo.

15. Mhariri wa gazeti la **Jicho Pevu** ametangazia wasomaji katika toleo la Jumatano kutuma makala

yao ili kuchangia katika kuandika tahariri itakayohusu mabadiliko ya hali ya anga na athari zake katika toleo la Jumapili. Andika makala yako